# TEACHER.CO.KE

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**KISWAHILI KARATASI YA TATU**

**KIDATO CHA NNE**

## SEHEMU A : FASIHI SIMULIZI (Lazima)

a)Utanzu – Hadithi (1x1)

Kipera – Ngano za usuli (1x1)

b)i)Fanani : paukwa

Hadhira : pakawa

ii)Fanani : Hadithi! Hadithi

Hadhira : Hadithi njoo

c)i)Huburudisha wanajamii husika

ii)Huelekeza wanajamii husika

iii)Huelimisha wanajamii husika

iv)Huhifadhira huziona ya jamii husika

v)Huonya wanajamii wa jamii husika

vi)Hujenga ushirikiano wa jamii husika

vii)Hujenga kumbukumbu ya wanajamii. **zozote (5x1)**

d)i)Huhusisha wahusika wanyama

ii)Wanyama hupewa tabia za binadamu

iii)Huwa na ucheshi mwingi

iv)Hutoa matumaini kwa wanyonge kwamba mwishowe watakuwa washindi

v)Hutoa maadili na kuonya kwa njia ya kuchekesha isiyoumiza. **Zozote 5x1**

**e)Umuhimu wa fomyula ya kutanguliza**

i)Humtambulisha mtambaji

ii)Huvuta makini ya hadhira

iii)Hutoa hadhira kutoka ulimwengu halisi hadi wa ubunifu

iv)Hutofautisha kipera cha hadithi na vipera vingine

v)Huashiria mwanzo wa hadithi

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes



For more FREE KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

vi)Hushirikisha mtambaji na hadhira. **zozote 3x1**

**FOMYULA YA KUHITIMISHA**

i)Hupisha shughuli nyinginezo

ii)Huashiria mwisho wa hadithi

iii)Hutoa funzo kwa hadithi

iv)Humpisha mtambaji mwingine

v)Hupumzisha hadhira

vi)Hutoa hadhira kutoka ulimwengu wa hadithi hadi ulimwengu halisi. **Zozote 3x1**

## SEHEMU B:TAMTHILIA YA KIGOGO ( PAULINE KEA)

**2 .** (a)

i. Maneno haya ni ya sauti ya mzee Kenga
ii. mawazoni mwa Majoka.
iii. Haya yanatendeka katika ofisi ya Mzee Majoka
iv. wakati Husda na Ashua wanapigana.
v. Majoka anakumbuka ushauri wa Kenga wa jinsi ya kumnasa Ashua kwa kusababisha fujo baina yake na Husda.

(b) Swali balagha – huoni ni fursa nzuri ya kulipiza kisasi?
Nahau – kummezea mate; kumtamani

(c )

i. Kumwaga kemikali na taka sokoni licha ya kuwa wananchi wanakaa na kufanyia biashara zao katika soko.
ii. Kuwatumia wahuni kunyamazisha wapinzani. Mzee Kenga anakutana na Wahuni chini ya mbuyu ambao baadaye wanamwumiza Tunu.
iii. Kuruhusu dawa za kulevya na wanafunzi ambao wanakuwa makabeji
iv. Kuwaua wapinzani, kama vile vijana watano walioandamana
v. Kuwatumia polisi kuwaua na kurushia waandamanaji risasi na vitoa machozi.
vi. Kuwanyima wafanyakazi haki, kama vile walimu na wauguzi wanaongezewa asilimia ndogo ya mshahara kasha kupandisha kodi.
vii. Utawala kuruhusu uuzaji wa pombe haramu kinyume na katiba, ambao umesababisha vifo na kufanya watu kuwa vipofu.
viii. Kufungulia biashara ya ukataji miti ilhai watu wanategemea miti hiyo kuboresha mazingira.
ix. Kufunga kituo cha runinga ya Mzalendo kwa kuonyesha mkutano wa Tunu na wapinzani wengine wa utawala.
x. Utawala kutumia vyombo vya dola kuwafukuza watu wanaoenda sokoni na kuweka ulinzi mkali licha ya kuwa ulikuwa uwanja wa umma.
xi. Kuwarushia wakazi vijikaratasi vyenye ujumbe hasimu wakitakikana wapahame mahali ambapo wamekuwa wakiishi kwa muda wote wa uhai wao.



Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

For more FREE KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

d.

i. Kenga anamshauri Majoka amwalike Ashua na Husda ili patashika itokee, naye Majoka apate jinsi atakavyolipiza kisasi kwa Sudi kwa kukataa kuchonga kinyago.
ii. Anamshauri Majoka atangaze kuwa maandamano ni haramu kisha anawamuru maafisa wa polisi watumie nguvu zaidi dhidi ya umma unaondoa maandamano.
iii. Majoka anakataa Suala la polisi kutumia nguvu zaidi lakini Kenga anamwambia "Acha moyo wa huruma….. Siasa na hisia haziivi kwenye chungu kimoja ndugu yangu.
iv. Anakubali pendekezo la Majoka la kufunga Runinga ya Mzalendo kwa kupeperusha matangazo ya mkutano moja kwa moja.
v. Kenga alihusika katika kupanga mauaji ya Jabali kwani Majoka anamsifu kwa kupanga hilo na hata wanapigishana Konzi
vi. Anaibua pendekezo la kumuua Chopi kwa kutofuata maagizo ya kumuua Tunu akisema, "Nafikiri Chopi lazima aende safari."
vii. Anamwambia Majoka kuwa si kweli kwamba watu watampigia Tunu kura na kusema, "Tunu hawezi kupigiwa hata!"
viii. Anapendekea kukusanya kodi ya juu na kukataa kuitumia vyema na kwa njia halali k.v. kutoa taka. 6x1

**SWALI LA 3 - KIGOGO**

- Unyakuzi wa mali ya umma – Majoka anaamua kulifunga Soko la Chapakazi ili kujenga hoteli ya kifahari.
- Ubinafsi – Majoka anavibomoa vibanda vya Wanasagamoyo na kupanga kujenga hoteli yake ya kifahari.
- Utepetevu/ukosefu wa uwajibikaji – wananchi wanalipa kodi lakini wanakosa huduma kusafishiwa soko na huduma za maji taka.
- Vitisho – Majoka anatisha kumfuta Kingi kazi
- Viongozi wamekosa maadili ya kikazi – Majoka anamrai Ashua mkewe Sudi ili aendeleze ufuska naye.
- Kuwatesa wapinzani – Tunu na Sudi wanateswa lakini wanaendelea kupigania mageuzi
- Kuvunja sheria – Majoka anampa Mamapima kibali cha kuuza pombe haramu ambayo ni kinyume na katiba
- Wizi wa kura –Majoka anasema kuwa hata wasipompa kura atashinda



Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes
For more FREE KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

Teacher.co.ke

- Ubaguzi katika utoaji wa kandarasi - kandarasi ya kuoka keki inatolewa kwa Asiya ambaye ni mke wa Boza
- Matumizi mabaya ya pesa za umma – pesa zinatumiwa katika shughuli za kuchonga vinyago
- Utawala wa kiimla na wa kutojali – Wanasagamoyo hawana usemi wowote; Majoka anasema kuwa atajenga hoteli watu wapende wasipende
- Mauaji ya kikatili – watu wasio na hatia wanauawa; Jabali
- Kuzwazulia watu wasio na hatia - Ashua anazuiliwa na Majoka bila kosa lolote
- Wanasagamoyo wanakabiliwa na unyonyaji – bei ya chakula kwenye kioski cha kampuni imepanda maradufu tangu soko lilipofungwa
- Kuwanyima wanasagamoyo haki ya kaundamana – wanaharamisha maandamano
- Unasaba – Majoka anamwajiri Kenga ambaye ni binamuye kama mshauri wake mkuu
- Viongozi wanatumia nafasi zao kuwaangamiza vijana - matumizi ya dawa za kulevya – wanfunzi katika shule ya Majoka Academy wadungana sumu ya nyoka
- Utapeli - Kuwaongezea walimu mshahara na wauguzi na kuongeza kodi
- Kurithisha uongozi – Majoka anapanga kutambulisha Ngao Junior kuwa kiongozi mpya mpya badala ya Wanasagamoyo kumchagua kiongozi wao
- Kuruhusu biashara ya ukataji wa miti.
- Matumizi mabaya ya vyombo vya dola – polisi wanatumiwa kuwatawanya waandamanaji.

**SEHEMU C: RIWAYA YA CHOZI LA HERI (ASSUMPTA K MATEI)**

**4.** a) Eleza muktadha wa dondoo hili (Alama 4)

**Haya ni mawazo ya Kiriri akiwa nyumbani kwake kabla ya kifo chake. Alikuwa anasumbuka kwa kuachwa na jamaa yake. Alikuwa ameachwa na mkewe ,Annette na wanawe ambao sasa walikuwa ughaibuni na walikataa kurudi nchini alikokuwa Kiriri hata baada yake kuwarai.**

b)Huku ukitolea mifano maridhawa, fafanua mbinu nne za kifasihi zinazojitikeza katika dondoo hili (Alama 4)

**Maswali ya balagha/mubalagha -Kipi kinachowavuta kuhamia ughaibuni?**

**-.....nchi za ughaibuni ni twenty-four-hour economies?**

**Sitiari -mzigo wa simanzi kurejelea huzuni aliokuwa nao Kiriri kwa kuachwa na jamaa yake.**

**-Mshahara mnono-kurejelea mshahara mkubwa.**



Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

For more FREE KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

**Uhaishaji/tashihisi- mzigo wa simanzi ulipokilemea kifua chake.**
**Kuchanganya ndimi- twenty-four-hour economies.**

(4×1=4)

c)Eleza changamoto inayomkumba msemaji katika dondoo hili

**(Alama 2)**

**Ukiwa/upweke- Kiriri aliachwa na mkewe Annette na wanawe ambao sasa walikuwa ughaibuni.**

d)Fafanua jinsi maudhui yanayojitokeza katika dondoo hili yameshughulikiwa kwingineko riwayani.

(Alama 4)

**<u>Maudhui ya upweke/ukiwa</u>**
**Lunga anaachwa na mkewe**
**Umu anachwa na kijakazi**
**Umu anaachwa na watoto wao wakembe ;Dick na mwaliko waliouzwa na kijakazi.**
**Umu anaachwa na babake,Lunga anapoaga dunia hata baada ya Mamake kumwacha babake alipokuwa akilala.**
**Ridhaa anaachwa na mwanawe Tila,Mkewe ,Terry na pia mkaza mwanawe na mjukuwe.**
**Selume anaondoka nyumbani kwa katika Msitu wa Heri baada ya kushutumiwa na jamii ya mumewe.**
**Mwangemi anawapoteza Mkewe na mwanawe. Hata anapokuwa katika nyumba yake kando ya bahari,anawawaza.**

**(Hoja 4×1)**

a) Fafanua umuhimu wa mandhari katika kuijenga riwaya hii kwa kurejelea Msitu wa Mamba

(Alama 8)

**Ukosefu wa vyoo**
**Ukosefu wa malazi/malazi**
**Ukosefu wa chakula**
**Ukosefu wa maji safi**
**Upweke**
**Magonjwa kama vile kipindupindu**
**Uharibifu wa mazingira(Lunga na wakaaji wengine katika Msitu wa Mamba kukata miti ili kuendeleza kilimo.**
**Ukimbizi wa ndani kwa ndani.** **(Hoja 4×1)**

**5. Eleza jinsi maudhui ya ufisadi yalivyoshughulikiwa katika riwaya ya Chozi la Heri.**

- Nyumba za maskini zinapobomolewa Tononokeni, mabwanyenye wanaanza kutoa milungula ili nyumba zao zisibomolewa.
- viongozi wanapowapoka raia ardhi zao, raia walalamikapo hupozwa roho kwa kuambiwa kuwa kumeundwa tume za kuchunguza kashfa hizo.
- wakati wa uchaguzi, wanasiasa wanawahonga raia ili wawachague. Papa aliwahonga kwa pesa na unga.
- Hazina ya Jitegemee inalenga kuwafaidi vijana wa taifa la Wahafidhina lakini ukabila na unasaba unapoliandama hawanufaiki.
- nyumba zinazolengwa kupewa maskini katika mtaa duni wa Sombera zinachukuliwa na viongozi baada ya ujenzi kukamilika.
- familia ya Bwana kute inajigawa na kuwa familia tatu ili wapate msaada mwingi kuliko wakimbizi wengine.
- Serikali inabomoa majengo ya raia katika mtaa wa Tononokeni na Zari bila kuwafidia.
- raia wanaiba mafuta ya lori ili wawauzie madereva wa wakubwa au walinda usalama ili wayauze kwingine.



Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

For more FREE KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

- madereva wa wakubwa wanafyonza mafuta kwa mirija na kuwauzia wenye magari ya kibinafsi.
- askari wananunua mafuta ambayo yameibiwa na kuyauza kwingine.
- matapei wanawauzia wananchi wenzao ardhi ya makaburi bila kujali
- raia matapeli wanauza ardhi zao mara mbili kwa watu wawili tofauti na kutoa hati miliki mbili halali na bandia
- viongozi wananyakua ardhi iliyotengewa upanzi wa chakula na kujenga nyumba zao mf. Madhabahu kwenye mlima wa Nasibu yalinyakuliwa ili kujenga hoteli za kitalii.
- vigogo wanauza mahindi yanayotolewa na mataifa ya nje kama msaada.
- vigogo wanawalazimisha wataalamu wa maswala ya lishe kuidhinisha uuzaji wa mahindi yaliyoharibika.
- viongozi wanapasua mbao na kuchoma makaa katika msitu wa mamba baada ya msitu huo kupigwa marufuku.
- viongozi wanahamisha wakimbizi kutoka msitu wa Mamba na kuanza kuvuna mahindi yaliyopandwa na wakimbizi badala ya kuwaruhusu kuyavuna kabla ya kuwaondoa.
- Baada ya Fumba kumpachika mimba mwanafunzi wake, aliachishwa kazi kwa muda kisha akahamishwa kwingine hivyo kumsababishia Rehema kutopata haki yake.
- Baadhi ya walinda usalama wanashirikiana na wahalifu ili wagawane mali iliyoibiwa.
- Magari ya vigogo hayaondolewi barabarani na askari licha ya kuwa mabovu.
- Buda anawahonga askari wanapoenda nyumbani kwake kumtia mbaroni.(biashara ya ulanguzi wa mihadarati) (Zozote 20x1=10)

## SEHEMU YA D:USHAIRI

### 6.SHAIRI LA KWANZA

(a) Bainisha bahari ya shairi hili ukijikita katika ruwaza zifuatazo (alama3)

(i) Mishororo

-Takhmisa –mishororo tano

(ii) Maneno

- Pindu-utao, mshororo wa mwisho wa ubeti unafanywa ukwapa wa mshororo wa kwanza ubeti unaofuata
- Kikwamba – Neno/ukwapi wa mshororo wa kwanza kila ubeti ni lile/yale yale

(ii) Vina – mtiririko

- Vina vyote, vya ndani vina urari (ni) aidha vina vya nche vina urari (ma)

(b) Eleza muundo wa shairi hili (alama4)

- Beti nane
- Mishororo 5 kila ubeti
- Bipande viwili kila mshororo
- Mizani kumi na sita kila mshororo
- Vina vya ukwapi ni ‘ni’ na vya utao ni ‘ma’
- Lina kibwagizo
-

(c) Bainisha mbinu zifuatazo za kimtindo katika shairi hili (alama3)

(i) Tashbihi –kidogo kama Sodom!

(ii) Taswira-uwaonapo fuoni, nusu uchi wa mnyama

Tasfida-wanatafuna maini (kushiriki ngano)



Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

For more FREE KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

(d) Eleza toni ya shairi hili (alama1)
- Kukashifu/kusuta/kushauri

(e) Bainisha nafsi nenewa katika shairi hili (alama1)
- Wanajamii

(f) Fafanua dhamira ya mtunzi wa shairi hili (alama2)
- Kukashifu utovu wa maadili katika jamii/mijini
- Kuonyesha uozo uliopo mijini

(g) Andika ubeti watatu kwa lugha tutumbi (alama4)
- Hakika, miji yetu imekuwa kama Sodoma.
- Watu hawana haya kwani wametupilia mbali maadhili
- Baba na binti zao hishiriki mapenzi wasichana wadog kuwa waja wazito. Miji yetu inafanana na Sodoma.

(h) Fafanua maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa na mshairi (alama2)
- Manani – Mola/Mungu
- Marijali-wasichana /mabinti

## 7.SHAIRI LA PILI

a) **Eleza dhamira ya shairi hili.** (al.2)
Anadhamiria kuonyesha wanyonge wanastahili usawa na haki – na wanyonge kupatiwa kwa bei kuzingatiwa bila kudhulumiwa – ubeti wa 4

b) **Baininsha tamathali mbili za usemi katika shairi hili.** al.2)
Tashbihi – ni kama la moto, wavitamani kama tama ya fisi
Takriri – Maendeleo ya umma
Nidaa – Lo!

c) **Eleza umuhimu tatu wa usambamba katika shairi hili.** (al.2)
Maendeleo ya umma (urudiaji wa fungu) – kusisitiza ujumbe
Urudiaji wa silabi …..ni, ki – kuleta ridhimu
Urudiaji wa neno.

d) **Onyesha jinsi maendeleo ya umma ulivyo kinaya.** (al.2)
Ni kinaya kuwa tuna vitu tele lakini bei I juu
Ni kinaya kuviona vitu madukani lakini kuvipata ng'o

e) **Eleza mambo ambayo mshairi nachukulia kuwa maendelo halisi ya umma.** (al.4)
Vitu kumilikiwa na wanyone kupiwa.
Bei kuzingatiwa bila kudhulumiwa
Dola kudhibiti vitu vijapo nchini mwetu.
Watu kuwa na kauli katika shughulika zao.
Watu kuwa waungwana.

f)**Tambua matumizi ya mstari mishata kwa kutolea mifano.** (al.2)
Mishororo ambayo si toshelezi katka shairi
Maendeleo ya umma

g) **Bainisha nafsi neni katika shairi hili.** (al.1)
Ni mzalendo/mwananchi-nchini mwet ubeti 5
Mtetezi wa haki – ubeti 4

h) **Fafanua toni ya shairi hili.** (al.1)
Kuhamasisha
Kuzindua



Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

For more FREE KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

i) **Andika ubeti wanne kwa lugha nathari.** (al.4)

Maendeleo ya umma ni kutafuta vitu na kuwauzia wanyonge kwa bei nafuu pasi na kunyanyasua wala kudanganywa na hivyo kulinda haki zao

7 a) **Wafanyikazi wa umma**

- Maskini na tajiri
- Wadogo na wenye vyeo.

b) **Inkisari -maendeleo , ndo/ndio**

Tabdila – Kutotowa /kutotoa

Kuboronga sarufi-Kujitegemea bora/bora kujitegemea.

c) Takriri neno-shuru ubet 2

takriri sialbi – vina katikati kila ubeti

d) **Mathnawi- vipande 2 kila mshororo**

Ukaraguni – vina vinabadilika ubeti hadi mwingine

Kibwagizo- mshororo wa mwisho umerudiwa kila ubeti .

Tarbia – mishororo 4 kila ubeti.

**a) Si vizuri kuomba misaada ya kigeni kila wakati.**

Hivyo ni sawa na kuwa mateka

Ni vyema kujitegemea kwa shida zetu

Taifa haliwezi kuimarika bila ushuru

**b) Maswali balagha - vipi wangalihudumu**

Jazanda /sitiari- twajifunga kamba/ kiguru

Tashbihi – ni kama kiguru

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes



For more FREE KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/